Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: *Toleo Na.39 - 2024*

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*




## Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023

## Sasa Rasmi



# BITEKO: Wazazi somesheni watoto

- KAZI IENDELEE -




**BODI YA UHARIRI**

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Veronica Chitunda
Nazareth Mwakabuta

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# TAHARIRI

## Tusipuuze kauli ya Prof. Nombo kuhusu kuthamini Elimu ya Watu Wazima

Elimu ya watu wazima ni kipengele muhimu ambacho hakiwezi kupuuzwa kama tunataka kufikia maendeleo ya kweli na endelevu hapa nchini. Hii inatokana na ukweli kwamba licha ya elimu hiyo kusaidia kuimarisha afya na ustawi wa jamii, pia inawapa wajifunzaji maarifa na ujuzi muhimu ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.



Zaidi ya hayo, elimu ya watu wazima ni nyenzo muhimu katika kuimarisha demokrasia na ushiriki wa raia, kwani inawasaidia watu kuwa na uelewa wa kutosha juu ya haki zao na wajibu wao kama raia na hivyo kuwa na ujasiri kushiriki katika shughuli za kijamii, hali hii inachochea dhana ya utawala bora.

Hata hivyo elimu ya watu wazima haijapewa kisogo, ndio maana Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza program mbalimbali zinazolenga kuongeza maarifa na ujuzi, na miongoni mwa programu hizo ni pamoja na Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule (IPOSA) ambayo mpaka sasa imefanikiwa kuwarejesha vijana 12,000 waliokuwa nje ya mfumo rasmi wa elimu.

Aidha programu nyingine zinazochagiza ujifunzaji ni Mpango wa Uwiano kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA) pamoja na Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Walioikosa (MEMKWA).

Kwa kuzingatia umuhimu wa elimu hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo aliasa kuwa tusiidharau elimu ya watu wazima, akisisitiza kuwa elimu hiyo ina mchango mkubwa katika kuwezesha wananchi kupata maarifa, ujuzi na mielekeo stahiki kwa maendeleo endelevu.

Kauli ya kiongozi huyo inapaswa kuzingatiwa, aidha kupuuza kauli hiyo ni sawa na kukosa kutambua mchango mkubwa ambao elimu hii inaweza kuleta katika kupunguza umasikini, kuongeza ajira, na kuboresha ustawi wa wananchi.


Ni wakati muafaka sasa jamii na wadau mbalimbali kushirikiana kuunga mkono juhudi za serikali kuhakikisha elimu hii inatiliwa mkazo na kupewa rasilimali zinazostahili.



Wazazi Someshe ni Watoto >



# Dkt. Biteko awataka wazazi kusomesha watoto wapate elimu



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewataka wazazi kutumia fursa ya miundombinu ya Shule ya Sekondari ya Miles and Kimbery White iliyojengwa kwa ufadhili wa Shirika la Abbot kuwasomesha Watoto ili wapate elimu bora.

Dkt. Biteko ametoa rai hiyo Oktoba 01, 2024 Mkoani Tanga akizindua miundombinu ya Shule hiyo iliyojengwa katika Kata ya Mapatano wilaya ya Mkinga mkoani humo kwa gharama ya zaidi ya shilingi Bilioni 12.

"Miundombinu imejengwa kwa gharama kubwa ni vema ikatunzwa na kuhifadhiwa ili iwe na manufaa kwa jamii na taifa kwa ujumla". Alisema Dkt. Biteko.

Aidha Mhe. Biteko amewahimiza wanafunzi kusoma kwa bidii na kuchukua tahadhari ya baadhi ya maudhui yanayopatikana katika mitandao ya kijamii, ili kuhakikisha wanafaulu vizuri mitihani.

Kwa upande wake, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda amepongeza Shule hiyo kuitikia wito wa kuwa Shule ya Sekondari ya Mkondo Amali, ikijikita katika amali ya kilimo.

Aidha Prof. Mkenda amesema Wizara imejipanga kusimamia mafunzo ya amali, ambapo shule zaidi ya 100 zitajengwa Nchi nzima na kwamba wanafunzi, watakaomaliza Sekondari mafunzo ya Amali watapata cheti za Kidato cha Nne na cheti cha VETA, na wanaweza kwenda kufanya kazi za ufundi sehemu yoyote.

Naye Mtendaji wa Mkuu wa ABBOTT, Robert Ford amesema Shule hiyo inakusudia kuwasaidia Watoto wa eneo hilo kupata elimu na ujuzi huku akiwashukuru wakazi wa eneo la Mapatano kwa ushirikiano walionesha katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi.

Ushirikiano Kuimarisha Elimu >



# Tanzania, Afrika Kusini kushirikiana kuimarisha Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amekutana na Waziri wa Elimu ya Juu Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Afrika Kusini Mhe. Dkt. Bonginkosi Nzimande ambapo wamejadili namna ya kuimarisha uhusiano katika nyanja za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

Waziri Mkenda ameeleza kuwa Tanzania inajivunia uhusiano mzuri na wa kihistoria na Afrika Kusini katika masuala mbalimbali ya kijamii ikiwemo Elimu, na kwamba ni muhimu nchi hizo kushirikiana katika nyanja hizo ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

Kwa upande wake, Dkt. Nzimande amepongeza Serikali ya Tanzania kwa kuchukua hatua mbalimbali katika kuongeza hamasa ya matumizi ya Sayansi na Teknolojia hasa katika dunia ya sasa inayobadilika kwa kasi.

Waziri huyo amesema kuwa Wizara hizo zimekubaliana kuendelea kushirikiana kufanya uwekezaji madhubuti katika Sayansi Teknolojia na Ubunifu ili nchi ziweze kufikia maendeleo.

Awali akizungumza Mkurugenzi Idara ya Sayansi na Teknolojia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Ladislaus Mnyone amesema ziara ya ujumbe huo inalenga kuchochea juhudi mbalimbali za kuongeza ukuaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kuboresha maisha ya Watanzania.



Ufadhili Elimu >



# Shule za Sekondari za Simiyu, Dodoma kufaidika na ufadhili kutoka KOICA

Shirika la Maendeleo la Korea Kusini (KOICA) linatarajia kutumia dola za kimarekani milioni 10 kufadhili mradi wa ujenzi wa maabara za kisasa za sayansi na TEHAMA katika shule za Sekondari mkoani Simiyu na Dodoma.

Hayo yamejiri Oktoba 28, 2024 nchini Korea Kusini, kufuatia ziara ya kimafunzo ya Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo iliyolenga uimarishaji mafunzo katika Nyanja za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati.



Prof. Nombo amebainisha kuwa Shirika hilo pia linatarajia kujenga Chuo Kikubwa cha Ufundi eneo la Kihonda mkoani Morogoro (Morogoro Polytechnic College) kitakachogharimu dola za kimarekani milioni 19.5.

''Hizi ni juhudi za Serikali chini ya Rais Samia zinazolenga kukuza na kuimarisha mafunzo ya Sayansi Teknolojia, Uhandisi na Hesabu (STEM) katika ngazi zote za elimu nchini ikiwa ni pamoja na kushirikiana na wabia wa maendeleo" alisema Prof. Nombo.

Aidha Nombo amesema Tanzania imedhamiria kukuza na kuimarisha mafunzo ya Sayansi Teknolojia, Uhandisi na Hesabu katika ngazi zote za elimu kwa kuwa na mbinu na mikakati stahiki pamoja na kuongeza wataalamu katika maeneo hayo na kuhimiza ushiriki wa wanafunzi wa kike.

Katika ziara hiyo Prof Nombo ameambatana na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Miko na Serikali za Mitaa ndugu Atupele Mwambene na Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania Dkt. Aneth Komba.

Ujenzi Shule za Kata >

# Serikali imejenga shule 760 za kata kati ya 1,000 nchi nzima kupitia SEQUIP





Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema kuwa Serikali inaendelea kuwekeza kwenye sekta ya elimu kwa kiasi kikubwa ili kuwezesha watoto wa kitanzania kupata elimu katika mazingira bora na kuwajengea ujuzi.

Waziri Mkenda ametoa kauli hiyo Oktoba 03, 2024 akizindua shule mpya ya Sekondari ya Nyombo iliyopo katika Kata ya Ikuna wilaya ya Njombe mkoani Njombe, akisisitiza kuwa jukumu lililobaki ni wazazi kuhakikisha wanawasimamia vema watoto na kufuatilia maendeleo yao.

"Rais Samia anaendelea kuhakikisha vitabu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya kisasa pamoja na kuboresha mazingira ya walimu" amesisitiza Prof. Mkenda.

Aidha, ameongeza kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatenga fedha kwa kila mwaka kwa ajili ya kutoa mafunzo kazini kwa walimu ili kuwawezesha fursa mbalimbali ikiwemo kubadilishana uzoefu katika masuala muhimu ya elimu ili kuinua viwango vya elimu.

Mbunge wa Jimbo la Lupembe Mhe. Enock Swale amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha maendeleo yanawafikia watu wa chini na kwani jimbo hilo lenye Kata 12 mpaka sasa lina Shule mpya 13 za Kata.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Nyombo Anastazia Nchemwa amesema kuwa zaidi ya shilingi Milioni 583 zimetumika katika ujenzi wa miundombinu ya shule hiyo.

Aidha amebainisha kuwa tayari Serikali imeshawapatia vitabu kwa ajili ya ujifunzaji na ufundishaji na kwamba jumla ya shilingi Milioni 100 imeshawekwa katika akaunti ya shule kwa ajili ya ujenzi wa nyumba pacha ya walimu.

Maoni Sheria ya Elimu >



# Wadau wasisitizwa kutoa maoni kuhusu Sheria ya Elimu

Mwenyekiti wa Kamati ya kukusanya maoni kwa ajili ya kufanya mapitio ya Sheria ya Elimu Prof. Eustella Bhalalusesa amesema wadau wana mchango mkubwa kwa katika zoezi hilo muhimu kwa taifa, hivyo wana jukumu la kushiriki kikamilifu katika kutoa maoni kuhusiana na changamoto zilizopo kwenye Sheria ya Elimu Sura ya 353.

Prof. Eustella amesema hayo Oktoba 31, 2024 jijini Dar es Salaam alipokuwa akizungumza baada ya kikao na wadau wa maendeleo akisisitiza kuwa, Serikali ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa Sera ya Sera ya elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023, kuna matamko mbalimbali ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi ili yaingie kwenye sheria ya elimu.

Nae Mkuu wa Kitengo cha Sheria Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Adv. Innocent Mgeta amesema kamati hiyo inaendelea na vikao vyake kwa kushirikisha wadau mbalimbali kufanya mapitio ya Sheria ya Elimu kuwezesha ufanisi katika utekelezaji wake.

Kwa upande wake Mshauri wa Elimu kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini Tanzania Dkt. John Lusingu amesema, kikao hicho kimewapatia nafasi ya kufahamu masuala mengi ikiwemo muundo wa elimu na majukumu mbalimbali ya Serikali katika kuendeleza, na kwamba ni jambo muhimu makundi hayo kushiriki kutoa maoni juu ya sheria ya elimu kwani ndio roho ya sekta hiyo.



Elimu ndani ya Mfumo Rasmi >




# Vijana 12,000 waliokuwa nje ya Mfumo Rasmi wa Elimu warejeshwa





Serikali imefanikiwa kuwarejesha katika mfumo rasmi wa elimu vijana wapatao 12,000 waliokuwa nje ya mfumo rasmi wa elimu.

Akizungumza katika Kilele cha Maadhimisho ya Kitaifa ya Juma la Elimu ya Watu Wazima Oktoba 11, 2024 mkoani Tabora Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu Ofisi ya Rais TAMISEMI Dkt. Emmanuel Shindika amesema kati ya waliorejeshwa wasichana ni 6,594 na wavulana 5,406.

Dkt. Shindika ameongeza kuwa vijana hao wamerejeshwa kupitia Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule (IPOSA) na kuwa wamefanikiwa kupata ujuzi katika fani mbalimbali ikiwemo kwa kutumia programu za kompyuta ambapo baada ya kuhitimu zimewawezesha kuingia katika ajira.

Awali akizungumza kwa niaba ya Kamishna wa Elimu, Mkurugenzi wa Elimu Msingi Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Maulid Mnonya amesema utaratibu wa kuwarejesha wanafunzi waliopata mdondoko ni hatua moja kubwa ya kupongeza Serikali kutokana na Waraka wa Elimu Namba 3 wa Mwaka 2021.

Ameongeza kuwa Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 imeelekeza elimu itolowe kwa watu wote, hivyo elimu ya Watu Wazima inalenga kujenga maarifa na ujuzi.

Mkurugenzi huyo amewataka Watanzania wote kuona fursa mbalimbali za elimu kwa walioikosa au waliopata mdondoko na kuzitumia kuwawezesha kufikia malengo yao ya elimu kupata ujuzi utakao wawezesha kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

Nae Afisa Mafunzo kutoka Shirika la Kimataifa la DVV Bw. Matteo Mwita amesema Shirika hilo linaendelea kushirikiana na Serikali katika kuboresha mifumo ya elimu ya Watu Wazima ili kuchochea maendeleo.

Ziara ya Kimafunzo>



# Kituo cha Elimu Maalum na masuala ya jinsia UDSM chaikosha Benki ya Dunia



Timu ya Benki ya Dunia imekipongeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kujenga Kituo kitakachosimamia masuala ya watu wenye mahitaji maalum na jinsia.

Akizungumza Oktoba 29, 2024 Jijini Dar es Salaam wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), Kiongozi wa Timu ya Benki hiyo Prof. Roberta Malee amesema amefurahi kuona maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho unaolenga kuifanya elimu ya juu kuwa sehemu salama na wezeshi kwa wanafunzi wote na kwamba kitakuwa mfano kwa nchi nyingine.

Mtaalam Mwandamizi wa Elimu kutoka Benki ya Dunia Nkahiga Kaboko amesema kituo hicho ni muhimu katika kutoa ujuzi na kuvijengea uwezo vyuo vingine ili kuboresha utekelezaji wa elimu ya juu jumuishi.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Jinsia Dkt. Lulu Mahai amesema kuwa kituo hicho kitawezesha UDSM kuwa mahali salama pasipo na ukatili wala unyanyasaji wa kijinsia na kuandaa wataalamu wa masuala ya kijinsia na Maendeleo ya Jamii.

Mwanafunzi wa Chuo hicho Mwenye mahitaji maalum ameishukuru Serikali kwani kupitia kituo hicho wanafunzi wote watapata elimu katika mazingira rafiki na bora

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mbali ya kujenga kituo hicho, pia kinajenga Kampasi mpya Mkoani Kagera na Lindi, majengo mapya katika kampasi Kuu ya Dar es Salaam na katika kampasi ya Buyu kupitia Mradi wa HEET.

Lishe na Elimu >

# Lishe bora inawezesha wanafunzi kitaaluma - Dkt. Lyabwene




Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Lyabwene Mtahabwa amesema lishe bora ni muhimu kwa wanafunzi kwani inawawezesha kuwa na afya njema kimwili na kuhamasisha kushiriki kikamilifu katika masomo.

Dkt. Lyabwene ameeleza hayo Oktoba 28, 2024 jijini Dar es Salaam akifungua kikao kazi cha wadau wa lishe shuleni kujadili na kuandaa mpango kazi utakaowezesha utekelezaji fanisi wa afua za lishe katika shule.

Aidha Kamishna huyo amesisitiza kuwa suala la lishe shuleni ni muhimu na linahitaji kujadiliwa kwa kina na wadau wote ili kuhakikisha kila mtoto anapata lishe bora akiwa shule.

"Ili wanafunzi waweze kujifunza vizuri wanahitaji mazingira mazuri pamoja na kuwa na afya bora ya kimwili na kiakili" alisema Dkt. Mtahabwa

Kikao kazi hicho kimehusisha wadau mbalimbali wakiwemo Wizara ya Elimu, Ofisi ya Rais Tamisemi, Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Wizara ya Fedha, Wizara ya kilimo, Wizara ya Afya, Wizara ya maji, Wizara ya Maendeleo ya jamii, Pamoja Tuwalishe na wadau wengine wa lishe nchini.



Utekelezaji Miradi ya Elimu >



# Utekelezaji mradi wa HEET wafikia asilimia 55, Benki ya Dunia yapongeza




Serikali imesema imeridhika na utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya kiuchumi (HEET) unaotekelezwa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini kuputia ufadhili wa Benki ya Dunia ambao umefikia asilimia 55 katika kipindi cha Miaka Miwili na Nusu ya utekekezaji.

Akizungumza Oktoba 20, 2024 Jijini Dar es Salaam baada ya kikao na Wajumbe kutoka Benki ya Dunia, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof Carolyne Nombo amesema kuwa Serikali imejidhatiti kuhakikisha Mradi huo unakamilika Kwa asilimia 100 kabla ya muda wa utekelezaji kuisha. Mradi wa HEET unalenga kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia pamoja na kuweka miundombinu bora katika Vyuo inayoendana mazingira ya sasa na inakayowezesha kuongeza fursa na kutoa mafunzo yanaendana na Mageuzi ya elimu na kuchagiza maendeleo ya kiuchumi nchini.

"Tupo katika hatua nzuri na karibu kila eneo la mradi limeguswa katika kipindi hiki cha miaka miwili na nusu ya utekelezaji mradi, na tunaelekea kukutana na wadau wote kufanya tathimini ya maeneo ambayo bado yanahitaji uangalizi wa haraka ili kufikia malengo kama ilivyokusudiwa" amesema Prof. Nombo.

Naye Kiongozi wa Ujumbe wa Benki ya Dunia Prof. Roberta Basset Malee amepongeza Serikali hasa katika usimamizi wa Mradi huo na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha unakamilika kama ulivyopangwa. Moja ya eneo kubwa la utekekezaji mradi huu ni ujenzi wa Kampasi 16 za Vyuo vikuu katoka mikoa mbalimbali nchini ikiwemo kikoa ya Kigoma, Mtwara, Njombe, Tanga na Mara.

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz